# EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD - TANZANIA

ASSEMBLIES OF GOD

EAGT

# MWONGOZO WA UTENDAJI KAZI EAGT

Infinix HOT30i

CamScanner

# EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD (TANZANIA) MWONGOZO WA UTENDAJI KAZI KATIKA KANISA LA (EAGT)

**UTANGULIZI:**
Tunamshukuru Mungu kwa kusajiliwa kanisa letu la EAGT Serikalini, Mungu amedhihirisha uaminifu wake kwetu sote akitutetea katika mapito mbalimbali na kutufikisha mahali ambapo tunaweza kumtumikia tukitambulikana kisheria katika nchi yetu.

Na kwa kuwa tumesajiliwa na kuwa na Katiba yetu inayotuweka katika utaratibu mzuri, Baraza la waangalizi lililokutana tarehe 28/11/1995 liliona upo umuhimu wa kuwa na mwongozo wa utendaji kazi ili kuepuka migongano.

Baraza hilo liliomba Kamati kuu itayarishe mwongozo huo na kuletwa kwenye kikao kitakachofuata ili kupitishwa. Hata hivyo, kwa kuwa Kanisa la EAGT linayo Katiba yake tayari, itambidi kila mchungaji ajipatie ya kwake ili kuoanisha mwenendo wa kanisa zima.

1. **MADHUMUNI YA MWONGOZO HUU:**
   a) Kupunguza kama si kuondoa kabisa utata unaoweza kuwepo kwa yeyote katika utekelezaji au utendaji wa kazi ya Mungu katika kanisa lake.

   b) Kuepuka migongano na maingiliano katika utendaji.

2. **KATIBA YA KANISA:**
   a) Kwa kuwa hatuwezi kuendesha shughuli za kanisa katika nchi yetu inayoongozwa kisheria bila katiba, imetubidi tuwe na katiba yetu inayoonyesha jinsi



EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD (TZ)
UFUFUO CHURCH KONGA
BOX 17129
DAR ES SALAAM

Infinix HOT 30i

CamScanner

tunavyoendesha kazi na imani yetu ilivyo au tuaminivyo

b) Popote palipo na watu wengi waliokubaliana kufanya jambo lolote lazima pawe na utaratibu ili kila mmoja afahamu mahali pa utendaji wake na mipaka yake

c) Kwa kuwa Mungu wetu ni wa utaratibu na watumishi wake wote wamchao kwa moyo safi wana utaratibu, na ni lazima kila mmoja aheshimu huo utaratibu kwa ajili ya utukufu wake Mungu.

## 3. NEMBO YA KANISA:

Kanisa lina Nembo yake kama alama ya kujitambulisha

a) Ni budi kila muumini wa kanisa hili aangalie anapochapisha nyaraka kuhakikisha inakuwa na sura ya Nembo iliyokubalika, mfano mzuri unaoonekana vema katika vitambulisho vya utumishi.


b) Makaratasi yanayochapishwa na kuwekewa Nembo (Headed Papers) yaonyeshe vitu vilivyomo kwa usahihi na chini ya karatasi hizo linawekwa andiko la kutoka kitabu cha Marko 16:15 ("Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe") lisiwe andiko lingine tofauti.

## 4. MISINGI YA IMANI:

a) Kila mchungaji ni lazima ajifunze vile tunavyoamini ili kujilinda na imani potofu.

b) Kila aliyeitwa kuwa mtumishi katika EAGT atapaswa kwenda shule ya Biblia:

EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD (T)
DAR ES SALAAM


ASKOFU MKUU
MAKAMU ASKOFU MKUU
MSHAURI MKUU
KATIBU MKUU
MHAZINA MKUU
ASKOFU WA KANDA
MAKAMU WA KANDA
KATIBU
MHAZINA
ASKOFU WA JIMBO
MAKAMU WA JIMBO
MHAZINA
KATIBU
MCHUNGAJI
WAZEE WA KANISA
MASHEMASI
WASHIRIKA



CamScanner

c) Ni wajibu wa kila mchungaji kumlea mtumishi yeyote anayeitwa na kuwa karibu naye kumwongoza ili kufikia kukamilika wito wake. Si busara muumini anapojieleza kwa mchungaji wake kuwa ameitwa mara moja kumkabidhi kazi, bali ajifunze huduma hiyo chini ya mchungaji wake au aende shule ya Biblia kwa mwaka mmoja wa pili akabidhiwe kazi wakati anaendelea kusoma na kulelewa na mchungaji wake.

5. **WADHAMINI:**
Kanisa lina wadhamini wanaosimamia umilikaji mali za kanisa kwa niaba ya kanisa wao ndio wenye mamlaka ya:

a) Kuandika barua juu ya kupata hati za kudumu za viwanja vyote pamoja na kuandika barua hizo ikibidi

b) Hata hivyo, kazi zao zingine zimeonyeshwa katika Katiba ya EAGT Ibara ya sita (IV) B 3

6. **VIKAO**
Ili kwenda na utaratibu wa kikatiba, lazima kama wewe ni kiongozi utapaswa kuangalia utaratibu wa vikao katika Ibara ya kumi na moja ya Katiba.

7. **UONGOZI KATIKA EAGT:**
Ni lazima kila mtumishi aujue uongozi wote wa EAGT kwa ngazi zote ili kumpa mwanga katika utendaji kazi vema, Uongozi uko kama ifuatavyo:

Ili kutoa picha kamili angalia mchoro huu hapa chini (organization chart) kuangalia ngazi zinavyoonesha kila mmoja mahali au nafsi yake.



Infinix HOT 30i

CamScanner

(b.1) MABARAZA / VIKAO
- i) KAMATI KUU YA EAGT
- ii) HALMASHAURI KUU YA EAGT
- iii) BARAZA KUU LA WAANGALIZI
- iv) MKUTANO MKUU

(b.2) i) KAMATI KUU YA KANDA
- ii) HALMASHAURI YA KANDA
- iii) MKUTANO MKUU WA KANDA

(b.3) i) KAMATI YA JIMBO
- ii) HALMASHAURI YA JIMBO
- iii) MKUTANO WA JIMBO

(b.4 i) BARAZA LA WAZEE / MASHEMASI
- ii) VIKAO VYA IDARA
- iii) KIKAO CHA KANISA LA MAHALI PAMOJA

8 (a) Kazi ya viongozi wa ngazi zote zimeonyeshwa katika Katiba pamoja na shughuli za mabaraza yote yaliyoonyeshwa hapo juu soma katiba Ibara ya kumi na moja (XI)

(b) Hata hivyo katika Katiba haionyeshi shughuli za Mshauri Mkuu.

**Shughuli za Mshauri Mkuu zitakuwa ni:**
- i) Kumshauri Askofu Mkuu na Makamu wake
- ii) Kuwa mjumbe wa Kamati kuu katika vikao vya kamati kuu
- iii) Mjumbe katika vikao vya Halmashauru kuu na Baraza la Waangalizi
- iv) Atawajibika kwa Askofu Mkuu.



EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD (TZ)
UFUFUO CHURCH - KONGA
P. O BOX 17129
DAR ES SALAAM

Infinix HOT 30i

CamScanner

## 9. UINJILISTI

Kwa ajili ya kuuleta ulimwengu kwa Yesu Kristo, tutakuwa na Wainjilisti wa aina nne kama ifuatavyo:

a) **Wainjilisti wa Taifa:**
Hawa ni wahubiri waliowekewa mikono kuhubiri mahali pote nchini na nje ya nchi baada ya kuthibitishwa kufanya vema toka ngazi ya chini, yaani Jimbo na Kanda.

b) **Wainjilisti wa Kanda:**
Hawa ni wale waliopandishwa baada ya kufanya vema katika huduma yao Jimboni na kupandishwa kwenda Kanda.

c) **Wainjilisti wa jimbo:**
Hawa ni wale walioonyesha huduma ya Uinjilisti katika Jimbo baada ya kuhudumu bila kutambuliwa katika ngazi yoyote ila kulingana na mzigo walio nao wamekuwa wanafanya mikutano na inaleta mafanikio kila waendako, hao jimbo linawatambua rasmi katika vikao vyao kuwaweka wawe wa jimbo.

d) **Wainjilisti wasiotambuliwa bado na jimbo:**
Hawa ni wale wanaotoka makanisani, wanaanzia mikutano wanayoandaa chini ya wachungaji wao na wanaonyesha matunda ya kiinjilisti na wana mwito huo.

**MUHIMU**:
Wainjilisti wote kama wengine wote walioitwa wathibitishwe kweli kwamba wanafaa kupandishwa ngazi iliyo mbele yao pia wanao wito huo.



CamScanner

***Mfano:*** Mwinjilist ni mvuna roho yaani anashughulikia roho zilizo gizani (watu wasiookoka ndio lengo lake)

10. **WAALIMU:**
Waalimu watakuwa na ngazi au wa aina 4 kama ilivyo kwa Wainjilisti na wataendelea kupanda kwa namna ile ile.

11. **MTUME:**
Mtume ni mtu aliyepewa huduma ya kuanzisha kazi mpya na anailea kwa muda kisha anamwachia mwingine kuichunga (yaani kanisa) naye pia ataendelea kupanda ngazi kama vile ilivyo kwa mwinjilisti

12. **MCHUNGAJI:**
Mchungaji ni mtu aliyeitwa kutunza roho zilizokombolewa, pia kuzitafuta zisizookolewa na kuhubiri Injili ya wokovu, ni mtumishi anayeingia ndani ya miyo ya watu kwa neno na maisha yao akijitolea kikamilifu kwa ajili ya kondoo.

13. **WAUMINI:**
a) Tunapozungumzia waumini tunamaanisha watu waliotubu dhambi zao kwa kumwamini Yesu Kristo na kumruhusu kuishi ndani yao na kuacha dhambi kabisa.

b) Hairuhusiwi kumpokea mtu anayetaka kujiunga kaitka ushirika bila toba,ila hatafukuzwa mtu yeyote anayeingia kanisani kusikiliza Neno la Mungu bali bali hatahesabiwa kuwa muumini au mshirika wa imani yetu, hatakuwa na haki yoyote kanisani.

14. **UANZISHAJI WA MAKANISA:**
Uanzishaji wa makanisa mapya utakuwa kama ifuatavyo:



Infinix HOT 30i
CamScanner

**b) Kukosa ufahamu.**

Kukosa ufahamu kujitambua hujui na hivyo hutafuti siri za Mungu na unakosa kuendelea kwa kuwa ulipo unaona umefika hivyo unabaki ulipo na kwa kuwa unaongoza watu wengine utawatesa kwa ufinyu wa mawazo na utendaji wako. Unapaswa kujiendeleza.

3. Migogoro inaweza kusababishwa na mambo mengi mbalimbali, lakini la muhimu ni uwezo wa kuitatua katika haki na kuleta amani ya kweli. Nitoe mifano michache ya migogoro.

a) Migogoro inayotokana na fedha

b) Kutotambua wakuongozao

**a) Jiepushe na tamaa ya fedha**

i) Awepo Mtunza Hazina wa kanisa, mchungaji kagua kwa wakati maalum Kujua taarifa za fedha zinaandaliwa vema.

ii) Unapohitaji fedha usijizoeze kuchukua, wakupatie watunzao na uzitumie kwa ajili ya kazi inayoeleweka.

iii) Michango yote mbalimbali itunzwe na Mtunza fedha wa kanisa (mahali pa kutunzwa si kanisani bali Benki).

**b) Utii**

i) Utii ni silaha mojawapo ya kushinda kiburi kama ulivyo unyenyekevu.

ii) Kila mtumishi atapaswa kuwatii walio juu yake kama Mungu aagizavyo.



nfinix HOT 30i

CamScanner

vi) Atapelekwa Jimboni na mchungaji wake ili apokelewe; Asikae sana chini ya kanisa mama labda ikiwa haendelei vizuri kanisa linalofikia kiwango kilichoelezwa katika kifungu cha pili asipitishwe miaka mitatu, apokelewe Jimboni.

vii) Matawi yanayoanzishwa na Jimbo yatakuwa chini ya Kamati ya Jimbo

## 15. MAPATO YA KANISA:

Angalia Ibara ya XIV ya Katiba

## 16. MIGOGORO KATIKA MAONGOZI:

Migogoro inaweza kusababishwa na mambo mawili makuu.

1. Kushuka ki - roho au kuanguka kabisa kiroho.

2. Kukosa ufahamu wa uongozi wa kiroho.

**a) Kushuka/kuanguka ki - roho.**

Kupoa kunasababisha mambo mengi yanayomchukiza Mungu, yanaweza yakatokea yafuatayo:-

i) Kiburi kwa kufaulu kazi au maisha ya mwili unakosa ulinzi wa Mungu kwakuwa hakuna unyenyekevu

ii) Kukosa utii huwezi kusikiliza mtu, huwezi kufundishwa/ kuelekezwa n.k

Infinix HOT 30i



CamScanner

a) Kutoka kanisa hadi kanisa pawe na umbali wa km 2 (mbili) na iwapo mji huo utakuwa na msongamano mkubwa wa watu, basi linaweza kuanzishwa kanisa umbali wa km $1^1/_2$ . Hata hivyo yawepo makubaliano na kanisa liliopo karibu juu ya uanzishaji huo.

b) Mwangalizi atawajibika kushauri kuanzishwa makanisa mahali panapofaa na atatumia taratibu za vikao vyake halali.

c) Makanisa yanayoanzishwa na kanisa mama. Makanisa hayo yatatambulikana kama matawi ya kanisa mama na yatalelewa na kanisa mama mpaka yafikie uwezo wa kujitegemea kama ifuatavyo:

i) Uwezo na msimamo mzuri wa imani yetu

ii) Yamefikia idadi ya waumini 15 - 30 wenye uwezo na wanaotoa zaka na sadaka na uwezo na kumtegemeza mtumishi anayewaongoza.

iii) Mtumishi anayewaongoza atatambulikana na mchungaji wake kama mkristo mtenda kazi na atapewa kitambulisho cha mamna hiyo.

iv) Atatoa zaka yake na kanisa lake kwa kanisa mama, mapato yanayobaki "ataruhusiwa kuyatumia na pia atatunza sehemu ya mapato kwa ajili ya shughuli za kanisa". Na iwapo zaka zitatosheleza kwa mahitaji yake ataacha kutumia sadaka za kawaida kwa ajili ya "bills "na wageni wa kanisa au ujenzi.

v) Atawajibika kwa mchungaji wake wa kanisa mama.



finix HOT 30i

CamScanner

c) **Kuwatambua wakuongozao:**
Kila anayeweza kuwa kiongozi mzuri na kukuza kiwango cha kuijenga kazi ya Mungu lazima awatambuwe walio juu yake.
1. Kwa kuwastahi/kuwaheshimu
2. Kutekeleza kwa uaminifu maelekezo wanayotoa.

## 17. YANAYOTOLEWA KATIKA VIKAO:

a) Maamuzi yote yanayopitishwa katika kikao chochote, hayajadiliwa tena na watekelezaji wa maamuzi hayo, kwa kuwa tayari yalishajadiliwa na kufikia maafikiano.

b) Wanaopewa kutekeleza majukumu yaliyotolewa katika vikao wanaposhindwa kutekeleza na kukosa kutoa sababu za kuridhisha, watapaswa kujiuzulu kusimamishwa uongozi wao kwa taratibu za kikatiba.

## 18. TARATIBU ZA VIKAO:

a) Kila kikao lazima kiwe na Mwenyekiti, Katibu na wajumbe.

b) Kila kikao lazima kiwe na Agenda ambazo zitapaswa kuletwa na Mwenyekiti au wajumbe na itapaswa zichujwe iwapo zinapaswa kuwa agenda au la.

c) Vikao vitaendeshwa kwa taratibu za kibunge. Zinatolewa hoja juu ya agenda zitaungwa mkono au kupingwa kwa kupiga kura za wazi au siri itategemea suala au agenda yenyewe.

i) Utaratibu huo Mwenyekiti sio msemaji bali wajumbe, yeye atamalizia.

Infinix HOT 30i



CamScanner

ii) Nafasi ya wanaochangia suala au agenda iwiane na idadi ya wajumbe wa kikao na nafasi iwepo ya kutosha kuchangia.

d) Lazima vikao vyote zitolewe miniti zake na kupewa wajumbe na moja itunzwe katika faili kwa ajili ya kumbukumbu za ufuatiliaji na utekelezaji. Kila kikao kitakachofanyika lazima kopi moja itumwe ofisi iliyo juu ya kikao hicho.

## 19. UANDISHI WA BARUA - KIKAZI:

Kila unapoanza kuandika barua utambue ngazi yako inayokuhusu kuandikia

**A. Mfano - Barua za kikazi za kawaida**

1. Mchungaji anayo haki kumwandikisha Askofu wa Jimbo moja kwa moja, hawezi kumwandikia Askofu wa kanda wala Askofu Mkuu.

2. Askofu wa jimbo: Atamwandikia moja kwa moja Askofu wa Kanda.

3. Askofu wa Kanda Atamwandikia moja kwa moja Askofu Mkuu

4. Kanisa la mahali pamoja: Halitamwandikia kiongozi yeyote bila kibali cha mchungaji wa kanisa hilo.

5. Barua yeyote itakayoandikwa na kanisa, kiongozi kwa kuruka ngazi, halitatambulikana, itakuwa ni batili au haitashughulikiwa.

## 19. B. BARUA ZIHUSIANAZO NA MIGOGORO

1. Barua zote zitaanzia kwa kufuata utaratibu ulivyo



ifinix HOT 30i
CamScanner

katika fungu "A"

a) Kama kuna mgogoro kati ya kanisa na mchungaji wazee wa kanisa watamwomba kikao, akikubali watazungumzia hapo, mchungaji akiwa Mwenyekiti,wakipatana yataishia hapo

b) Wakishindwa kupatana watamwomba mchungaji wamwite Askofu wa Jimbo akikubali, watamwandikia Askofu barua na nakala watampa mchungaji wao Akikataa watalazimika kumwita tu Askofu na watampa nakala ya barua mchungaji wao.

2. Askofu akishindwa ataiambia kamati yake, ikishindwa ataita Halmashauri ya Jimbo ikishindwa watalipeleka suala hilo kwa Askofu wa Kanda Kanda ikishindwa watalipeleka kwenye kamati Kuu.

3. Kamati kuu ikishindwa, italipeleka mbele, mwisho itaishia Baraza Kuu la Waangalizi Hata hivyo hekima ya Mungu itakuwa imemaliza hasa tukizingatia.Neno la Mungu toka (Yakobo 3:13 -18)

## 20. MAENDELEO YA KANISA LA MAHALI PAMOJA

### A. Maendeleo ya Ki - roho

Ni wajibu wa viongozi wa ngazi zote kuanzia mchungaji wa kanisa la mahali pamoja kuhakikisha kanisa linakuwa KIROHO SIO KIMWILI.

1. Mchungaji wa mahali pamoja, atapaswa kuutumia muda wake wote kwa kazi ya Mungu, atakuwa anaomba na kulihudumia Neno, ona mfano katika Mdo 6.4 walivyo shughulikia mambo makuu mawili.



Infinix HOT 30i

CamScanner

3. Wasimamizi wa miradi

i) Mchungaji ataweka kamati za miradi watakao husika kuiendesha yeye atakuwa mshauri na mkaguzi mkuu pamoja na kuhakikisha inaendelea katika njia salama.

ii) Miradi itakuwa na hawa wafuatao:-

a) Mwenyekiti
b) Katibu
c) Mtunza Hazina na wajumbe

## 21. KUHAMA KWÀ WATUMISHI TOKA KANDA MOJA KWENDA NYINGINE

a) Hatuna uhamisho katika EAGT.

b) Kuhama kutatokana na hiari ya mtumishi mwenyewe aonavyo uongozi wa Mungu katika moyo wake

c). Anapotaka kuhama kutoka Kanda moja kwenda kanda nyingine atatakiwa kuwasiliana na Askofu wake wa jimbo ambaye atamwandikia barua kwa Askofu wake wa Kanda yake na Askofu wa Kanda atampa barua ya kanda kwenda nayo Kanda nyingine, na nakala ya barua hiyo itaenda ofisi ya Kitaifa.

d) Mtumishi anapokelewa na Kanda anayohamia ofisi ya Kanda hiyo itampeleka ofisi ya Jimbo na kumtambulisha katika vikao mbele ya Halmashauri ya Jimbo.

- Watumishi hawatapokelewa kwa kuhama kienyeji bila taratibu hizo.

e) Kuhama toka jimbo hadi jimbo: Mtumishi atapewa barua na Askofu wa jimbo kwenda kwa Askofu wa jimbo



Infinix HOT 30i

CamScanner

analohamia rasmi na kumtambulisha kwa wachungaji katika vikao vyake vya kawaida. Jimbo analohamia litampokea rasmi na kumtambulisha kwa wachungaji katika vikao vyake vya kawaida

## 22. UTUMISHI KWENDA NCHI ZA NJE

### a) MASOMO:

Atatakiwa kupata kibali toka kwa Askofu wake wa Jimbo na Kanda na atatakiwa kuonyesha Prospectus kuangalia iwapo chuo aendacho kusoma kinakubalika au kulingana na imani ya kanisa la EAGT. Kujua hayo atapaswa kuwasiliana na Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo. Kisha akipata hicho kibali cha nje atatakiwa akiombe toka Kamati kuu.

### b) KUTEMBEA:

Mtumishi anayetaka kwenda nchi za nje kutembelea tu kama mapumziko, atatakiwa apate vibali toka kwa Askofu wake wa Jimbo na Kanda na mwisho Kamati Kuu.

## 23. KUPOKEA WAGENI TOKA NCHI ZA NJE

### A: KI - MISIONARY

Mgeni yeyote kutumika na EAGT kama Mmisionari (MTUME) atapaswa kuwasiliana na Kamati kuu ya EAGT sio na kanisa la mahali pamoja au mtumishi. Mmisionari wa kanisa la mahali pamoja hatakubaliwa kwa usalama wa makanisa.

### B: MGENI RAFIKI

Kama kanisa au mchungaji atakuwa na rafiki mgeni toka nje ya nchi, ili akubalike kutoa huduma katika Kanisa EAGT itabidi Askofu wa Jimbo na Kanda ajue na akubali na Kamati kuu ijulishwe.



inix HOT 30i

c) Mchungaji mjumbe wa Halmashauri yoyote ya Kanisa. Atapokelewa na mchungaji mwenyeji anapokwenda kutoa huduma yake.

d) Mtumishi yeyote kuondoa wakristo wa kawaida

i) Hataruhusiwa kufikia kwa mkristo afike kwa mtumishi aliyepo hapo aendapo

ii) Ikiwa ana ndugu na angependa kufikia hapo atatakiwa kutoa taarifa kwa mchungaji aliye karibu ili afahamu.

e) Kama ni mjumbe wa Kamati ya Jimbo, atapokelewa na mchungaji na baraza lake la kanisa ikiwezekana na kanisa na atahudumiwa na kanisa husika.

## 2. MAPATO YA TOKANAYO NA HUDUMA:

Mapato ya sadaka ya huduma anayofanya kuondoa zaka na sadaka ya Jumapili asubuhi atapewa mhudumu huyo bila kupunguzwa

## 3. SAFARI ZA WAUMINI

a) Wakristo wanaposafiri kibinafsi wanapaswa kuaga kwa mchungaji na kupewa barua ya safari na wasifikie kwa mchungaji huko waendako.

b) Wanaposafiri kwa shughuli za kanisa watapokelewa na kanisa na kupata huduma hapo kulingana na utaratibu uliowekwa kanisani hapo.

Nchi Jirani idhini itatolewa na jimbo kwa pamoja na kanda (wapewe taarifa ) hiyo, mtumishi imani yake na Dhehebu.

## 24. SAFARI ZA KIKAZI ZA WATUMISHI NGAZI ZOTE: SAFARI ZA KIOFISI (KUTEMBELEA AU KUTATUA MATATIZO)

**A: Wajumbe wa Kamati Kuu**
Watapokelewa na ofisi ya Kanda na kuwaandalia huduma zote wakati wote watakaokuwepo hapo.

**B: Wajumbe wa Kamati ya Kanda**
Watapokelewa ofisi ya Jimbo na kutayarishwa huduma zote za wakati wote atakaokuwepo.

**C: Wajumbe wa Kamati ya Jimbo**
Watapokelewa na mchungaji na baraza lake la kanisa na atayarishiwe huduma zote wakati wote atakaokuwepo hapo kikazi.

### 1. SAFARI ZA KIHUDUMA

Huduma hapa ni kama vile Uinjilisti, Semina n.k

a) Kama mtumishi huyo ni mjumbe wa Kamati Kuu. Atapokelewa na Ofisi ya Kanda na Jimbo na kanisa husika atakapotoa huduma na kanisa litahusika na huduma zote.

b) Kama mtumishi huyo ni mjumbe wa Kamati ya Kanda. Atapokelewa na Ofisi ya mchungaji na Baraza lake la Kanisa. Na atahudumiwa na kanisa husika huduma zote.



EVANGELISTIC ASSEMBLIES OF GOD (TZ)
UFUFUO CHURCH UKONGA
P.O BOX 17129
DAR ES SALAAM

Infinix HOT 30i

CamScanner

a) **Kuomba:** Walijadili na kuwa na muda wa kutosha katika maombi na kwa kufunga. Kutunza uhai wa kiroho na kukuza uweza wa Mungu ndani ya maisha yao ya utumishi.

b) Walihubiri Neno: Hawakuwa na porojo madhabahuni, walitoa neno lenye kuumba, kwa sababu walijilisha Neno hilo wenyewe. Ili uweze kuwa na kanisa hai (lenye nguvu za Mungu),lazima hayo mawili yafanywe kwa nguvu zote.

2. Viongozi (Maaskofu) Watahakiksha au watashughulikia kuhakikisha makanisa yaliyo katika majimbo yao yanakua kiroho na kuongezeka katika idadi ya wanaookolewa na kufanya mapenzi ya Mungu kwa nguvu.

3. Viongozi katika mahali pamoja, hawatawekwa kwenye uongozi wowote mpaka wamejazwa na Roho Mtakatifu, usiweke mzee au shemasi asiyejazwa Roho Mtakatifu au hajabatizwa katika maji mengi.

4. Hapatakuwa na Mzee kiongozi, anatosha mchungaji.

**B. Maendeleo ki - maisha**

1. Kila mtumishi wa Mungu pamoja na kuwahudumia waongofu ki - roho, ni wajibu wake kuhakikisha pia wanafanya kazi kwa bidii, kwa ajili ya mahitaji yao na kwa kazi ya Mungu. Mchungaji awafundishe kutenda kazi kwa ajili ya mahitaji yao kila siku (UVIVU NI DHAMBI).

2. Ikiwezekana kanisa pia liwe na miradi ya kujiendeleza.



inix HOT 30i

CamScanner

ASSEMBLIES OF GOD

EAGT

CS CamScanner